

## HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

OFISI YA MKURUGENZI  
MJI WA KIBAHAS.L.P 30112, KIBAHA  
SIMU Na: 023 - 2402886  
FAX No: 023 - 2402007

Kumb.Na. KTC/LD/PT/19546/9

26/03/2023

Kamishna wa Ardhi Msaidizi  
Mkoa wa Pwani  
S.L.P 9230,  
**DAR ES SALAAM.****YAH: HISTORIA YA VIWANJA NAMBA 250&251 KITALU 'A' ENEO LA  
MISUGUSUGU BAMBA- KIBAHA MJINI.**

Tafadhali husika na kichwa cha barua hapo juu.

Kihistoria eneo tajwa hapo juu lilikuwa likimilikiwa kimila na kampuni ya **YMDY CO. LTD** ya S.L.P 2040 **DAR ES SALAAM** kama ilivyothibitishwa na serikali ya mtaa wa **MISUGUSUGU** (muhtasari wa kikao umeambatanishwa). Awali eneo hili lilikuwa linamilikiwa na ndugu **STEPHEN AUGUST** ambaye baadae aliuzua eneo hilo kwa ndugu **YAN YANLI** S.L.P 2040 **DAR ES SALAAM** ambaye pia ni mkurugenzi wa kampuni ya **YMDY CO. LTD** kwa gharama ya USD. Mia moja Hamsini na nane elfu mia nne (158,400.00) tu (mkataba wa mauzo umeambatanishwa) na kwamba taratibu zote za kuhamisha miliki hiyo ya kimila zilifuatwa.


Kampuni ya **YMDY CO. LTD** ya S.L.P 2040 **DAR ES SALAAM** ilitayarisha mchoro wa mipangomiji namba **31/76/092009C** kwa matumizi ya **VIWANDA VYA HUDUMA** yaani **SERVICE TRADE INDUSTRY** na upimaji ulifanyika na kukamilika kwa kupewa namba ya ramani **E'354/732** na kusajiliwa kwa namba **191935**.

Kampuni ya **YMDY CO. LTD** ya S.L.P 2040 **DAR ES SALAAM** iliwasilisha kivuli cha cheti cha usajili wa kampuni pamoja na memorandum ya kampuni na baada ya kupitia kumbukumbu hizo ilibainika kuwa wakurugenzi wa kampuni sio raia wa Tanzania hivyo walitakiwa kuwa na kibali (*Certificate of Incentive*) chini ya kifungu namba **17** cha Sheria ya Uwekezaji namba **26** ya mwaka **1997** na walitimiza sharti hilo kwa kupewa certificate no. **022441136**.

Kwa kuwa wamiliki wa kampuni husika ni rala wa kigeni, baada ya kukamilisha taratibu za makabidhiano na mmiliki wa asili nimeatayarishia *Land Form no. 1* kwa ajili ya kutenga ardhi husika kuwa ardhi ya uwekezaji chini ya kituo cha uwekezaji kama sheria inavyoelekeza.

Baada ya taratibu husika za kuitangaza ardhi hiyo kukamilika, kiwanja hiki kimilikishwe kwa *Tanzania Investment Centre* ambao watatoa *Derivative Right* kwa **YMDY CO. LTD** kama sheria inavyoelekeza.

Nakutakia kazi njema.



Kennedy Mpanduji  
Kny: MKURUGENZI WA MJI  
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA